

ODA YA JANGA YA MDHHS DIS. 18




Vizuizi katika hudhurio kwa mikusanyiko ya makazi.

NDANI: HADI WATU 10 KUTOKA NYUMBA 2


NJE: HADI WATU 25 KUTOKA NYUMBA 3

- Barakoa zinahitijika kila wakati, isipokuwa wakati wa kula au kunywa.
- Wakaazi wanapaswa kufuatilia [miongozo ya mikusanyiko salama ya kijamii](#) ya MDHHS na wanahimizwa kutengeneza [“podi” ya watu](#) kushirikina nao mara kwa mara.



Vizuizi katika hudhurio katika sehemu zisizo za makazi.

NDANI



- Mikusanyiko ya ndani katika sehemu zisizo za makazi zimepigwa marufuku, isipokuwa kwa idadi kidogo ya ruhusa maalum, kama sehemu za kazi, au wakati mteja na mfanyakazi wanakusanyika ili mteja apate huduma.
- Walakini, sehemu nyingi bado ziko wazi kwa watu binafsi au nyumba moja.
 - Kila mtu ni sharti avae barakoa.
 - Maeneo yanapaswa kupangwa kuweka futi 6 ya umbali halisi kati ya nyumba nyingine.
 - Vipimo vya idadi maalum zinazigatiwa kulingana na maeneo



NJE

- Mikusanyiko ya nje ya hadi watu 25 inayofanyika katika maeneo yasiyo ya makazi yanaruhusiwa kama ifuatavyo:
 - KWA UKAAJI USIOGEUKA: zuia hudhurio hadi kwa kiwango cha asilimia 20 ya ukaaji.
 - BILA UKAAJI WAKUGEUKA: zuia hudhurio hadi kwa watu 20 kwa kila futi mraba 1,000, ikiwemo ndani ya maeneo ya wilaya katika nafasi ya tukio.
 - Kila mtu ni sharti avae barakoa.

“Mkusanyiko” inamaanisha tukio ambapo watu wawili au zaidi kutoka kwa nyumba moja wanapatikana katika nafasi ya kutumiwa kwa pamoja. Vile vile, mikusanyiko ya muda mfupi (kama vile duka, kituo cha ndege, sehemu ya huduma ya chakula) haija jumuishwa.

Barakoa bado zinahitajika.




Biashara, ofisi za serikali, shule, mashirika ya utunzaji wa watoto, wasafirishaji wa umma, na waratibu wengine wa mikusanyiko ni lazima wasilkubali mikusanyiko ya ndani au nje isipokuwa kama watu watavaa barakoa. Mashirika haya hayapaswi kudhania kwamba mtu anayeingia kwa biashara bila barakoa ameruhusiwa; lakini wanaweza kukubali uwakilishi wa matamshi ya mtu ambaye havai barakoa kwa sababu amepokea ruhusa maalum.

Rejareja na huduma za kibinafsi




- Mikusanyiko katika duka la rejareja, maktaba au makumbusho, haipaswi kupitisha asilimia 30 ya jumla ya idadi ya kiwango. Nafasi za ulaji wa ndani, ikiwemo sehemu za chakula, ni sharti zifungwe.
- Mikusanyiko ya kupata huduma za utunzaji wa kibinafsi, ikiwemo huduma za nywele, kucha, ngozi, kukanda, spa, tattoo, sanaa ya mwili, na utoboaji zinakubaliwa kupitia miadi, ikiwa tu huduma hio haihitaji utoaji wa barakoa.



Starehe na burudani

- Maeneo yafuatayo ya starehe na burudani yako wazi kufurahiwa na watu binafsi au nyumba moja ya hadi watu 6: ukumbi; uwanja; sinema; jumba la tamasha; maeneo ya uigizaji; maeneo ya michezo; viwanja; thieta; sehemu ya kupiga upinde; bustani za burudani; tao; jumba za bingo; sehemu za kuvingirisha mipira; kasino zisizo na ukabila; na sehemu za kulenga shabaha kwa bunduki.
 - KWA UKAAJI USIOGEUKA: zuia hudhurio hadi asilimia 20 ya kiwango cha ukaaji.
 - BILA UKAAJI WAKUGEUKA: zuia hudhurio hadi kwa watu 20 kwa kila futi mraba 1,000, ikiwemo ndani ya sehemu yeyote ya wilaya katika sehemu ya tukio.
 - Chakula na vinywaji haziruhusiwi kuuzwa au kutumiwa.
 - Kila mtu ni sharti abaki amevaa barakoa kila wakati.
 - Nyumba ni sharti ibaki na nafasi ya umbali wa futi 6 kutoka nyingine.
 - Idadi ya jumla katika kila chumba inazuiwa kuwa hadi watu 100, isipokuwa viwanja na ulingo, inayozuiwa hadi kwa 250.
- Mikusanyiko hayaruhusiwi katika maeneo ya hatari ya juu kama maeneo ya ulengaji kutumia leza; vilabu vya usiku; vilabu vya kutoa nguu; bustani ya maji; na bustani ya trampoli.



Huduma ya chakula

- Ulaji wa ndani katika baa na mikahawa haikubaliwi. Hii inajumuisha ulaji ndani ya ua zilozibwa sana, roshani, hema, na miundo mengine, isipokuwa ikiwa ziko wazi hewani. Tazama [Picha ya Ukaaji Nje](#) kwa taarifa zaidi.
- Huduma ya chakula kwa ulaji nje na usafirishaji inakubaliwa.
- Ulaji wa nje unakubaliwa ikiwa tu sio zaidi ya watu 6 wamekaa katika kila meza na meza zimewekwa umbali wa futi 6.
- Ulaji kwa nyumba ya waeskimo, kibanda, au kibanda kidogo inakubaliwa ikiwa tu ni familia moja tu iliyo ndani.



Zoezi, uhodari, na michezo

- Mikusanyiko inakubaliwa kwa madarasa ya zoezi na shughuli ya vikundi vya nje, na michezo ya nje yasiyo na mgusano.
- Mikusanyiko haikubaliwi kwa shughuli za zoezi za uhodari za ndani kama yoga, densi, kuendesha baiskeli, na mazoezi, wala kwa zoezi au burudani za mgusano wa karibu kama bustani ya trampoli na bustani ya maji.
- Zoezi la kibinafsi na mafunzo ya 1:1 inakubaliwa kwa vyumba vya mazoezi, vituo vya zoezi, na studio za zoezi.
 - Hudhurio haipaswi kuzidi asilimia 25 ya kiwango cha juu kwa jumla cha matumizi.
 - Ni lazima kuwe na umbali wa angalau futi 12 kati ya kila kituo cha kazi kinachotumika.
- Zoezi za kibinafsi, mafunzo ya 1:1, mafunzo ya kuongelea inakubaliwa katika vidimbwi vya ndani na nje.
 - Hudhurio haipaswi kuzidi utumizi wa kiwango kupita asilimia 25.
 - Sehemu za vidimbwi vya familia, bustani za maji, na sehemu zingine za mchezo zisizopangwa zinaweza kutofunguliwa.
- Zoezi za kibinafsi na mafunzo ya 1:1 inakubaliwa kwa utelezaji kwa barafu na kwa gurudumu.
 - Hudhurio haipaswi kuzidi watu 2 kwa kila futi mraba 1,000 (takriban watu 34 katika barafu mara moja katika sehemu ya kuteleza ya kawaida).
 - Kuteleza kwa barafu wazi/kwa kikundi na michezo isiyo ya mgusano zinakubaliwa kwa utelezaji barafuni wa nje.
- Michezo ya ndani na michezo ya mgusano, ikiwemo michezo ya shule ya upili na vyuo; michezo ya klabu; ligi za burudani za watoto, vijana, na watu wazima; na mashindano na matukio ya ufadhili; hayaruhusiwi hadi pale utakapo onyesha uzingatiaji wa [utaritibu ulioboreshwa wa upimaji na miongozo ya udhibiti wa maabukizi](#), ambayo inahitaji siku 6 kwa wiki kwa upimaji, hakuna mgusano wa kijamii aina yeyote na wanahadhira nje ya wanatimu wenzako na wana nyumba, na usimamizi kupitia wafanyakazi wa timu ya matibabu.